FRIEDRICH EBERT STIFTUNG

Tanzania Office

# Kuimarisha Mfumo Jumuishi wa Uteuzi wa Wagombea ndani ya Vyama vya Siasa Nchini Tanzania

Na
Consolata Sulley
University of Dar es Salaam
Desemba 2020

https://tanzania.fes.de

# Utangulizi

Vyama vya siasa vimekuwa viungo muhimu katika mfumo wa demokrasia shirikishi. Huibua, hutafuta na kuteua wagombea kwa ajili ya nafasi za kisiasa na za uongozi. Namna uteuzi wa wagombea unavyofanyika huashiria aina ya demokrasia ndani ya chama cha siasa. Katika kutekeleza majukumu yao ya kuteua wagombea, vyama vya siasa Afrika na hasa Tanzania vimeshindwa kuwapa wanawake nafasi wanayostahili kuwa nayostahiki. Kwa mfano, kati ya wagombea 11,933 waliogombea nafasi za urais, ubunge na udiwani mwaka 2015, wanawake walikuwa 904 tu (asilimia 7.5%).[1] Kwa hakika, asilimia ya wanawake wanaogombea imekuwa ikipungua kadiri wanapopanda ngazi za uongozi wa kisiasa. Ingawa wanawake walikuwa asilimia 53 ya wapigakura wote mwaka 2015, lakini walijumuisha asilimia 7.5 tu ya wagombea wote, na asilimia 5.4 ya wagombea walioachaguliwa.[2]

Kwa kutambua umuhimu wa vyama vya siasa katika kuhakikisha uwepo wa uwakilishi wa kutosha wa wanawake, Shirika la FriedrichEbert-Stiftung (FES) ofisi ya Tanzania iliona haja ya kufanya utafiti kwa lengo la kuchambua taratibu za uteuzi wa wagombea ndani ya vyama. Utafiti huu ulichambua taratibu za uteuzi ndani ya Chama cha Mapinduzi (CCM); Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA); Alliance for Change and Transparency (ACTWazalendo) na Chama cha Wananchi (CUF). Kwa kupitia uchambuzi wa sheria za vyama na za nchi pamoja na mahojiano na wadau mbalimbali[3], utafiti huu ulibaini udhaifu mkubwa ndani ya vyama na kwenye sheria za nchi pamoja na taratibu za uteuzi zisizozingatia usawa wa kijinsia. Kipekee zaidi, utafiti ulibaini matatizo kadhaa yanayokwamisha uteuzi wa wagombea wengi wanawake:

[1]Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), 2016. Ripoti ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi ya mwaka 2015 kwa ajili ya uchaguzi wa Urais, Ubunge na Udiwani. Dar es Salaam: Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali uk. 4345

[2]bid uk. 7275

[3]Viongozi wa vyama, maofisa na wagombea, Mamlaka za Usimamizi wa uchaguzi, Kituo cha Demokrasia, na makundi ya kiraia

## POLICY BRIEF

© Friedrich-Ebert-Stiftung
Ofisi ya Tanzania, 2020

Haki zote zimehifadhiwa. Hakuna sehemu yoyote ya chapisho hili inayopaswa kuzalishwa bila ruhusa ya mchapishaji isipokuwa nukuu fupi kwenye chapisho au hakiki muhimu. Kwa maelezo zaidi , andikia Shirika la Friedrich-Ebert-Stiftung Ofisi ya Tanzania.

Mwandishi anawajibika na maoni yaliyoandikwa kwenye chapisho hili. Maoni haya sio lazima yaakisi msimamo wa Friedrich-Ebert Stiftung Ofisi ya Tanzania.

Friedrich Ebert Stiftung, Ofisi ya Tanzania

P.O. Box 4472

Dar es Salaam, Tanzania.

- Mapungufu katika mifumo ya sheria za nchi na kitaasisi kwa kushindwa kuvilazimisha vyama vya siasa kuzingatia usawa wa kijinsia kwenye taratibu zake za uteuzi wa wagombea;
- Udhaifu wa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa wa kushindwa kuvisimamia vyama vya siasa kuzingatia usawa wa kijinsia;
- Ukosefu wa mikakati mahususi na inayojitosheleza ya kuhakikisha kuwa vyama vya siasa vinazingatia na kusimamia sheria na taratibu za ndani zinazozingatia uwepo wa misingi ya utu, usawa, haki, demokrasia, na uwazi;
- Mchakato wa uteuzi usio wazi na unaohodhiwa na mamlaka kuu za vyama na hivyo kuwatenga wanawake jambo ambalo limejidhihirisha katika vyama vyote vinne vilivyofanyiwa utafiti
- Mfumo dume, mazingira ya kisiasa yasiyo rafiki, viwango vya chini vya elimu, kukosa uzoefu wa uongozi, na ukosefu wa fedha ni vikwazo vikuu vinavyowafanya wanawake kuonekana hawana sifa za kuwa viongozi.

# Mapendekezo

Usawa wa kijinsia na ushiriki wa wanawake kwenye masuala ya uongozi na maamuzi bado ni changamoto kubwa duniani. Hata kama hakuna mwongozo wa jumla wa kushughulikia changamoto za uchache wa wanawake katika nafasi za uwakilishi, taratibu na mazoea ya utendaji ndani ya vyama ni masuala muhimu katika kuhakikisha kuwa kuna usawa wa kijinsia kwenye siasa na ngazi za maamuzi. Kwa hakika, mikakati ya kuwezesha kufikia usawa wa kijinsia itahitaji kuwepo hatua mahususi na za kutekelezwa na serikali na ngazi zote za vyama vya siasa. Ifuatayo ni mikakati ambayo vyama vya siasa, serikali na wadau wengine wanaweza kuitekeleza kwa ajili ya kuhakikisha kuwa usawa wa kijinsia unazingatiwa kwenye michakato ya kisiasa. Mikakati hii haiwezi kujitosheleza na kuwa mwarobaini wa vikwazo vyote vilivyoelezwa hapo juu. Kwahiyo, muktadha wa kisiasa, mgawanyo wa madaraka na maslahi ndani ya mfumo wa kisiasa na masuala mengine muhimu yote kwa pamoja yataweza kuchangia katika kufanikiwa au kutofanikiwa kwa mikakati hii.

***Kuzipitia na kuzifanyia marekebisho sheria zote zinazosimamia vyama vya siasa na uchaguzi ili kuvilazimisha vyama vya siasa kuzingatia usawa wa kijinsia na kuwahamasisha wanawake kushiriki chaguzi za ngazi ya kitaifa.***

Serikali inaweza kuasili mfumo wa mgawanyo wa wagombea (LCQ). Sheria hii ya mgawanyo wa kijinsia ikipitishwa basi itavilazimisha vyama kuhakikisha vinatenga walau asilimia 30 ya nafasi za uteuzi za wagombea ubunge na udiwani zitakazozingatia jinsia zote na pale ambapo vyama vitakiuka hilo vipewe karipio. Karipio linaweza kuwa katika

mfumo wa adhabu au faini kama vile kukatwa asilimia fulani ya ruzuku kwa vyama visivyozingatia masharti ya sheria hii, pamoja na kutoa motisha ya kuwaongezea ruzuku vyama vitakavyofanikiwa kuongeza kiwango cha idadi ya wanawake wagombea. Matakwa haya ya kisheria na karipio kuhusiana na makosa hayo vimefanya kazi vizuri nchini Burkina Faso ambako sheria ya mgawanyo wa wagombea kwa misingi ya kijinsia ilitungwa mwaka 2009 na kuanza kutumika mwaka 2012. Kifungu cha 5 na 6 cha sheria hiyo ya mgawanyo wa kijinsia inaeleza kuwa "chama kitaorodhesha wagombea wake na kati ya hao asilimia 30 lazima iwe ni wanawake ama la watakabiliwa na adhabu".[4] Kati ya wagombea 7,036 walioshiriki uchaguzi wa wabunge wa Burkina Faso wa tarehe 29 Novemba, wagombea 2,040 (asilimia 29) walikuwa wanawake".[5] Uwakilishi wa wanawake uliongezeka kutoka wanawake 17 kati ya wagombea 111 mwaka 2007 hadi wanawake 24 kati ya wagombea 127 mwaka 2012; ongezeko ni la kutoka asilimia 15.30 hadi asilimia 18.89.[6] Ongezeko hilo dogo linatokana na udhaifu kwenye sheria ya mgawanyo ya Burkina Faso ambayo haijajikita katika matokeo ya uchaguzi, bali inataka walau asilimia 30 ya wagombea iwe imegawanywa kwa jinsia zote mbili, inaangalia zaidi orodha ya wagombea. Kwa maneno mengine, sheria hailazimishi uwepo wa mgawanyo wa kijinsia wa wagombea kwenye vyama vya siasa. Kwahiyo, vyama vingeweza kuandaa orodha za wagombea zinazozingatiamgawanyo wa jinsia zote mbili, ingawa uwepo wa orodha hizo orodha si uhakika kuwa mwishoni mgombea wa jinsia fulani atachaguliwa.[7] Mfumo wa kuwa na orodha ya wagombea ambao wote watapigiwa kura kwa lengo la kuwa na uwakilishi wa kijinsia ni mwafaka kwa ajili ya kuleta ufanisi wa mfumo wa mgawanyo wa kijinsia.

## *Kufanya mapitio na marekebisho ya mfumo wa uchaguzi.*

Uzoefu unaonesha kuwa wanawake wana nafasi kubwa ya kuchaguliwa kupitia mfumo sawia wa uwakilishi (PR) au mchanganyiko kati ya mfumo sawia wa uwakilishi na mfumo wa uwakilishi kwa kulingana na wingi wa watu. Sheria inayopendekezwa ya kuwa na mgawanyo wa lazima wa kijinsia inaonekana kufanya kazi vizuri zaidi endapo kuna mfumo sawia wa uwakilishi au mifumo mchanganyiko kuliko ule wa 'anayeshinda huchukua kila kitu' kama huu unaotumika Tanzania. Kwa mfano, Afrika Kusini haina

[4]Tazama NDI (National Democratic Institute for International Affairs) & UNDP (United Nations Development Programme). 2012. Empowering Women for Stronger Political Parties: A Guidebook to Promote Women's Political Participation; IFES [International Foundation for Electoral Systems]. 2015. Elections in Burkina Faso: November 29 General Elections, Frequently Asked Questions. Arlington: IFES. (hakuna tafsiri kwa Kiswahili)

[5]United States Department of State. 2015. Country Reports on Human Rights Practices for 2015: Burkina Faso 2015 Human Rights Report. Bureau of Democracy, Human Rights and Labor.

[6]Gender Quota and Representation in Bukina Faso: Gender Quota Law, a small step forward. TransSaharan Election Project https://tsep.africa.ufl.edu/gender-quotas-and-representation/burkina-faso/. Imepakuliwa tarehe 19 Septemba 2020.

[7]Ibid.

mfumo wa mgawanyo wa lazima wa kijinsia au viti maalumu kwa ajili ya wanawake, lakini ndiyo nchi yenye idadi kubwa ya wabunge wanawake wanaochaguliwa kupitia mfumo sawia wa uwakilishi kupitia chama cha siasa. Kwa takwimu za mwaka 2013, nchi ya Afrika Kusini ilikuwa na asilimia 42 ya wabunge wanawake. Nchi nyingine zenye mfumo sawia wa uwakilishi ambazo zina wabunge wengi wanawake ni pamoja na Rwanda8 (64%), Shelisheli (mchanganyiko) (44%); Msumbiji (PR) (39%); na Senegali (mchanganyiko) (44).9 Mfumo unaotumika Afrika Kusini ni ule wa kubadilishana kati ya jinsia mbili. Kwa maana ya kwamba hakuna jinsia ambayo itakuwa juu kwenye orodha au nyingine kuwa ya mwisho. Ibara ya 76 ya Katiba ya Rwanda ina mchango mkubwa katika kuleta mgawanyo wa nafasi za uwakilishi kwa ajili ya wanawake. Rwanda inatupa mfano unaoonesha kuwa utaratibu wa uchaguzi unavilazimisha vyama vya siasa kuwateua wanawake kwenye nafasi muhimu.10 Mabadiliko ya sheria ya uchaguzi ya mwaka 2010 nchini Senegali yanalazimisha uwepo wa mgawanyo sawa kati ya wagombea wanaume na wanawake kwenye vyama vya siasa.

## *Kutengeneza upya mfumo wa majimbo ya uchaguzi kutoka mfumo wa sasa wa kila jimbo kuwa na mbunge mmoja hadi kuwa na wabunge zaidi ya mmoja ambapo kila jimbo litakuwa na mbunge mwanaume na mwanamke.*

Utaratibu huu utawezekana hata kwa nchi kama ya Tanzania yenye mfumo wa 'mshindi anachukua kila kitu'. Zaidi ya hayo yote, ilipendekezwa ndani ya rasimu ya katiba mpya ya mwaka 2014 iliyowasilishwa kwenye Bunge Maalumu la Katiba na Tume ya Kurekebisha Katiba, maarufu kwa jina la Tume ya Warioba kwa ajili ya kuridhiwa na kuongezewa mapendekezo zaidi.[11] Endapo mfumo huo utafanya kazi basi utaweza kuleta usawa wa kijinsia kwa asilimia hamsini kwa hamsini bungeni.

## *Kutunga na kuasili mfumo wa hiyari wa kuwa na mgawanyo sawa wa nafasi za wagombea.*

Vyama vya siasa nchini Tanzania vinatakiwa kupitia na kurekebisha sheria, kanuni na taratibu kwa ajili ya kuhakikisha kuwa vinatekeleza na kusimamia masuala ya usawa

[8]Rwanda ina sheria inayoelekeza kuwa lazima kuwepo na asilimia 30 ya viti maalumu na mgawanyo wa nafasi za ubunge kwa kuzingatia mfumo sawia wa uwakilishi. Mchanganyiko huu huenda ndo unaoifanya nchi ya Rwanda kuongoza duniani kwa kuwa na wanawake wengi kwenye nafasi za kiasa na utawala.

[9]International IDEA [Institute for Democracy and Electoral Assistance]. 2013. Political Parties in Africa through a Gender Lens. Asilimia hizi ni kwa mwaka 2013.

[10]Ahikire Josephine. 2009. Women's engagement with political parties in contemporary Africa: Reflections on Uganda's experience. Policy brief 65. Johannesburg: Centre for Policy Studies.

[11]Tazama "Ibara ya 113 (3) ya Rasimu ya Katiba Mpya ya Tume ya Warioba". 2014. Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali. Dar es Salaam, Tanzania.

wa kijinsia na sheria zinazohusu usawa wa kijinsia. Vyama vya siasa vinaweza kutunga na kuasili mfumo wa hiyari wa mgawanyo wa kijinsia kwa kuzingatia asilimia kwenye nafasi za uongozi na uteuzi wa wagombea. Uwepo wa sheria mahususi zinazohusu usawa wa kijinsia na kanuni zake ndani ya katiba za vyama na kanuni za usawa wa kijinsia utaweka mazingira wezeshi na kutengeneza utamaduni wa kukuza usawa wa kijinsia. Utaratibu mzuri zaidi ni ule wa mfumo wa hiyari wa chama tawala cha Afrika Kusini cha African National Congress (ANC) ambapo chama hicho kilitenga asilimia 50 kwa 50 ya viti vya ubunge kwa ajili ya wanawake na wanaume.12 Chama cha ANC kimeweka mfumo wake wa mgawanyo wa kijinsia, kwa kuhamasisha mgawanyo wa 50/50 kwa wanawake na wanaume. Utaratibu huu wa ANC umevishawishi vyama vingine kubuni mfumo kama huo wa kuongeza nafasi za uwakilishi za wanawake, hata hivyo vilivyo vingi havijaweza kufikia kiwango hiki cha ANC.13 Hali kadhalika, Ushelisheli haina sheria ya mgawanyo wa kijinsia, vyama vikuu kama vile Seychelles National Party (SNP) vimejiwekea utaaratibu wao wa hiyari unaosisitiza mgawanyo wa asilimia 33 kwa ajili ya wanawake kwenye Kamati Kuu ya Kitaifa pamoja na Mkutano wa Mkuu wa Taifa.

### *Vyama vya siasa ni vyema vikaasili mfumo wa mgawanyo wa nafasi za uongozi na kushiriki.*

Kwa njia hii, wapiga kura watakuwa na wawakilishi wa jinsia zote ili jinsia moja isitawale maamuzi muhimu ya ndani ya chama yakiwemo yanayohusu uongozi na uteuzi wa wagombea. Njia mojawapo ya kutekeleza hili ni kuasili sera ya ukomo wa jinsia kwa kuweka ukomo wa asilimia 40 ya mgawanyo wa kijinsia kwenye nafasi za uongozi wa ndani ya vyama. Sera hiyo siyo tu itaweka mazingira wezeshi kwa wagombea wanawake kwenye vyama, bali pia itapigania uwepo wa wanawake kwenye nafasi za maamuzi kwenye vyama vyao na hivyo kuchangia katika uteuzi wa wagombea utakaoleta uwiano wa kijinsia. Huko Sweden, miongoni mwa jitihada zake za kupambana na chama tawala cha Social Democratic, mnamo mwaka 1972 chama cha Kiliberali kilipitisha rasmi uamuzi wa kuhakikisha kuwa wanawake wanakuwa asilimia 40 ya viongozi wote ndani ya chama, ikiwemo Kamati Kuu.[14] Mwezi Februari mwaka 2019, vyama vinne kati ya nane vilivyoko ndani ya Bunge la Sweden (Riksdag) viliongozwa na wanawake. Mbali na hilo, tarehe 1 Februari 2019, Swedeni ilikuwa nchi ya tano duniani kuwa na wawakilishi wengi wanawake kwenye Bunge la Taifa ambapo asilimia 47.3 ya wabunge 349 walikuwa wanawake.

[12]African Women in politics: Miles to go before parity is achieved. African Renewal AprilJuly 2019_ https://www.un.org/africarenewal/magazine/april-2019-july-2019/african-women-politics-miles-go-parity-achieved imepakuliwa tarehe 15 Septemba 2020.

[13] Ibid

[14]International IDEA [Institute for Democracy and Electoral Assistance]. 2005. Women in Parliament: Beyond Numbers. A Revised Edition. Stockholm: International IDEA.

Kiwango hiki kinaifanya nchi ya Sweden kuongoza barani Ulaya.[15] Mfano huu wa Swedeni unatukumbusha usawa wa kijinsia kati ya wanaume na wanawake kwenye ngazi za maamuzi, ni mchakato wa muda mrefu na unahitaji kuwa na hatua endelevu. Mafanikio ya wanawake wa Swedeni kwenye uwakilishi wa kisiasa kwenye ngazi za maamuzi yanahusishwa moja kwa moja na hatua ya kuwajumuisha wanawake kwenye nafasi za maamuzi ndani ya vyama ambayo yameleta usawa wa kijinsia na uwiano mzuri wa uteuzi wa wagombea ndani ya vyama.

Tatizo mojawapo lililobainishwa kuhusu utaratibu wa kuwapata wagombea kwenye vyama vilivyofanyiwa utafiti ni la nguvu za mfumo wa tabaka la juu la uongozi na lililo na viongozi wanaume wanaodhibiti utaratibu mzima. Endapo hakutakuwa na utashi wa kisiasa wa uongozi ndani ya chama wa kupigania usawa wa kijinsia, basi mchakato wa uteuzi wa wagombea utatawaliwa na matashi ya wanaume na hivyo kupendelea jinsia moja na kukandamiza nyingine. Kwahiyo, mchakato wa kidemokrasia na shirikishi wa kuwateua wagombea unapaswa kuakisi mgawanyo wa viongozi ndani ya chama kwa ajili ya kuhakikisha kunakuwepo na uwanda sawa wa kufanya siasa pamoja na usawa wa kijinsia ndani ya vyama. Hili linaweza kufanyika kwa kutunga sheria ndani ya chama inayolazimisha uwepo wa angalau asilimia 30 ya wanawake kwenye maamuzi ya ngazi zote za chama. Hili limeweza kufanya kazi Rwanda ambako ipo sheria inayolazimisha mgawanyo wa kijinsia wa nafasi za uongozi katika ngazi zote za vyama vya siasa ikiwemo asilimia 30 ya wanawake.[16] Kiwango kikubwa cha wanawake kwenye vyombo vya maamuzi na ngazi za utawala kitaongeza fursa za wanawake kuteuliwa kama wagombea kwenye majimbo ya uchaguzi.

***Vyama vya siasa viimarishe nafasi na ushawishi wa umoja wa wanawake wa vyama katika kufanya maamuzi muhimu ndani ya vyama, kupigania ushirikishwaji wa wanawake na masuala ya jinsia kwa mujibu wa Kifungu cha 6A (2) cha Sheria ya Vyama vya Siasa (Maboresho) ya mwaka 2019.***

Umoja wa wanawake kwenye vyama vya siasa utakuwa na mchango mkubwa wa kutoa nafasi za uongozi kwa wanawake, kuwapa uzoefu na kuwajenga kiuongozi, kwakuwa haya ni mambo yanayozingatiwa zaidi wakati wa uteuzi wa wagombea. Umoja wa wanawake utawasogeza wanawake wanaotarajiwa kugombea machoni mwa viongozi wa chama, kuwashawishi na kuwavutia viongozi wa chama wanaopitisha maamuzi ili watenge nafasi kwa ajili ya wanawake kushiriki kwenye uongozi na kutunga sera ndani ya vyama.

[15] Inter-Parliamentary Union (IPU). (2019). Women in national parliaments: situation as of 1st February 2019. Imepakuliwa tarehe 31 Agosti 2020 kutoka http://archive.ipu.org/wmn-e/classif.htm.

[16] International IDEA [Institute for Democracy and Electoral Assistance]. 2013. "The status of women's structures within the parties". Political Parties in Africa through a Gender Lens.

***Vyama vya siasa vyenye sifa ya kupokea ruzuku ya serikali vinaweza kwa hiyari au kwa kulazimishwa na sheria kutenga asilimia 30 ya ruzuku zake pamoja na asilimia 10 ya bajeti ya kila mwaka kwa ajili ya kuwasaidia kifedha wagombea wanawake.***

Kiasi kitakachotengwa kielekezwe moja kwa moja kwenye mfuko wa uchaguzi kwa ajili ya wagombea wanawake au kipelekwe umoja wa wanawake kwa ajili ya mfuko maalumu wa uchaguzi wa wagombea wanawake. Uamuzi huo utawapa wanawake nguvu ya kifedha mara watakapoamua kugombea nafasi za uchaguzi.

***Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa (ORPP) iwezeshwe kisheria na kitaalam kwa ajili ya kuwa na nguvu za kuvilazimisha vyama vya siasa kuzingatia usawa wa kijinsia.***

Kufanyike mapitio ya sheria na zitekelezwe ili kuipa hadhi Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ya kuwa mdhibiti mwenye nguvu ya kusimamia michakato ya ndani ya vyama vya siasa, kwakuwa hilo ndo jambo la muhimu zaidi ambalo ofisi hiyo inapaswa kufanya

***Kuhimiza elimu kwa umma kuhusu usawa wa kijinsia kwenye vyama vya siasa na jamii ya Tanzania kwa ujumla kwa ajili ya kutekeleza mapendekezo ya hapo juu.***

Kampeni hizi za kutoa elimu kwa umma ni za muhimu kwa ajili ya kutokomeza ubaguzi wa kijinsia na dhana potofu dhidi ya wanawake kwenye michakato ya kisiasa pamoja na maisha ya kijamii. Jitihada kama hizi zitapunguza hali ya wanawake kutengwa kijamii, kiuchumi na kisiasa na kuongeza ushiriki wa wanawake kwenye siasa.